JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Anwani ya simu: 'SIASA'
Simu: 026 2137232
Fax: 026 2136924
Tovuti: www.orpp.go.tz
Parua Pepe info@orpp.go.tz

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja Vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi
Mtaa wa Nzuguni A
P.O. Box 2851
**DODOMA**

## TAARIFA KWA UMMA

## KIKOSI KAZI CHA KUPITIA HOJA ZILIZOJITOKEZA KATIKA MKUTANO WA WADAU WA DEMOKRASIA YA VYAMA VINGI VYA SIASA ULIOFANYIKA TAREHE 15, 16 NA 17 DESEMBA 2021 DODOMA

Washiriki wa mkutano wa wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa uliofanyika tarehe 15, 16 na 17 Desemba 2021 Dodoma, waliazimia kuunda kikosi kazi cha kupitia hoja zilizojitokeza katika mkutano huo na kuandaa mapendekezo yatakayowasilishwa kwenye Baraza la Vyama vya Siasa, ambalo litayapitia na kuyawasilisha Serikalini.

Aidha, walikubaliana pia kuwa, kikosi kazi hicho kijumuishe wawakilishi wa makundi yote ya wadau waliohudhuria mkutano huo na Msajili wa Vyama vya Siasa akapewa dhamana ya kuunda Kikosi kazi hicho, kwa kuwa anawafahamu vyema wadau hao. Vilevile, ilielezwa kuwa, Kikosi kazi hicho kifanye kazi hiyo na kuikamilisha ndani ya mwezi mmoja.

Hivyo, kwa dhamana niliyopewa na mkutano wa wadau tajwa hapo juu, nimeteua wajumbe wanaounda Kikosi kazi hicho, ambao wanajumuisha Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe kama ifuatavyo:-

| Na. | Jina na Wasifu | Wadhifa katika Kamati |
|---|---|---|
| 1. | Profesa Rwekaza S. Mukandara<br>Mwenyekiti wa Research and Education for Democracy in Tanzania (REDET), Mahadhiri Mwandamizi wa Sayansi ya Siasa Chuo Kikuu cha Dar-es salaam na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar-es salaam Mstaafu | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Hamad Rashid Mohamed<br>Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Siasa ADC na Waziri Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Sisty L. Nyahoza<br>Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa | Katibu |
| 4. | Prof. Bernadeta Kilian<br>Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar-es salaam-Utafiti. | Mjumbe |
| 5. | Prof. Alexander Makulilo<br>Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma-Taaluma. | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Amina Salum Ali<br>Mwenyekiti wa Bodi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Waziri Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Haji Omari Heri<br>Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Waziri Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Juma Ali Khatib<br>Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Mwenyekiti wa Kamati ya PAC ya Baraza la Wawakilishi | Mjumbe |
| 9. | Ndugu Christina Mndeme<br>Naibu Katibu Mkuu CCM Bara | Mjumbe |
| 10. | Ndugu Zitto Zuberi Kabwe<br>Mwenyekiti wa Tanzania Centre for Democracy (TCD) na Kiongozi wa chama cha siasa ACT-Wazalendo) | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Ndugu Abdul Mluya<br>Katibu Mkuu chama cha siasa DP na Mwakilishi wa vyama vya siasa visivyo na uwakilishi Bungeni. | Mjumbe |
| 12. | Ndugu Saumu Rashid<br>Mwakilishi wa viongozi wanawake wa Vyama vya Siasa. | Mjumbe |
| 13. | Shekih Alhadi Mussa Salum<br>Mwenyekiti wa Kamati ya Amani ya Kitaifa ya Viongozi wa Dini | Mjumbe |
| 14. | Mchungaji George Fupe<br>Makamu Mwenyekiti Kamati ya Amani ya Kitaifa ya Viongozi wa Dini | Mjumbe |
| 15. | Ndugu Anne Kulaya<br>Mwakilishi wa AZAKI zinazojihusisha na kupigania haki za wanawake. | Mjumbe |
| 16. | Mwakilishi wa AZAKI zinazopigania haki za wanawake Zanzibar (Jina lilatolewa baadaye) | Mjumbe |
| 17. | Ndugu Deodatus Balile<br>Mwenyekiti Jukwaa la Wahariri Tanzania na mwakilishi wa wanahabari. | Mjumbe |
| 18. | Mwakilishi wa AZAKi zinazopigania haki za watu wenye ulemavu Tanzania Bara (Jina lilatolewa baadaye) | Mjumbe |
| 19. | Mwakilishi wa AZAKI zinazopigania haki za Watu Wenye Ulemavu Tanzania Zanzibar (Jina lilatolewa baadaye) | Mjumbe |
| 20. | Ndugu Martin Mng'ong'o<br>Mwakilishi wa AZAKI zinazojihusisha na masuala ya siasa | Mjumbe |
| 21. | CP Benedict Wakulyamba<br>Mwakilishi wa Jeshi la Polisi | Mjumbe |
| 22. | Profesa Edward Hosseh<br>Rais wa Tanganyika Law Society (TLS) | Mjumbe |
| 23. | Slim Abdallah<br>Rais wa Zanzibar Law Society (ZLS) | Mjumbe |

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kikosi kazi kitasaidiwa na Sekretarieti ambayo itaongoziwa na Katibu. Wajumbe wa Sekretarieti watateuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa. Kila muhusika katika Kikosi kazi pamoja na Sekretarieti atapewa barua rasmi ya uteuzi. Aidha, kwa waajiriwa zitaandikwa barua kwa waajiri wao ili kuwaombea ruhusa.

Kwa lengo la kwenda na muda uliopangwa, Kikosi kazi kinatarajiwa kuanza kazi tarehe 10 Januari 2022, hivyo wahusika wote wanapaswa kuwa tayari kwa kazi kuanzia siku hiyo.

Kikosi kazi kitapewa hadidu za rejea ambazo zitakabidhiwa kwa Mwenyekiti wa Kikosi kazi siku ya uzinduzi wa Kikosi kazi hicho tarehe 10 Januari, 2022.

Nawatakia Wajumbe wa Kikosi kazi, kazi njema na Kazi Iendelee.

Jaji Francis S.K. Mutungi
**MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**
23 Desemba, 2021